

# CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE



## TANGAZO

### LA KUJIUNGA NA

### MAFUNZO YA UONGOZI NA MAADILI

Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), kinapenda kuwatangazia kuwa kutakuwa na Mafunzo maalumu ya Uongozi na Maadili yatakayofanyika kwa muda wa wiki moja. Lengo la Mafunzo haya ni kuwajengea uwezo washiriki katika stadi za Uongozi, Maadili na utawa bora na kuwajenga katika misingi imara ya Uongozi bora, uwajibikaji na uzalendo katika taasisi zao za Umma na binafsi kwa manufaa ya taifa la Tanzania.

#### **Malengo mahususi ya Mafunzo**

- i. Kujenga uelewa wa nadharia ya maadili na utawala bora na misingi ya utumiaji wa uelewa huo katika maeneo ya kazi.
- ii. Kuboresha weledi wa washiriki katika kutatua migogoro na kufanya makubaliano ya kidiplomasia sehemu za kazi.
- iii. Kuendeleza uwezo wa kufanya maamuzi kama viongozi na kupanua kiwango cha uelewa wa maadili na utawala bora kwa Washiriki.

#### **Walengwa**

Watumishi, Viongozi tarajiwa pamoja na Viongozi walio katika nyadhifa mbalimbali za kiuongozi katika taasisi za umma na binafsi.

#### **Muda wa Masomo**

Mafunzo yataendeshwa kwa muda wa wiki moja ambapo Mshiriki atachagua awamu moja kati ya nne kama ifuatavyo:

<b>Tarehe ya kuanza</b>	<b>Tarehe ya kumaliza</b>	<b>Mahali</b>	<b>Cheti kitakachotolewa</b>
3/5/2021	7/5/2021	Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam	Cheti cha Mafunzo ya Uongozi
2/8/2021	6/8/2021	MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam	Cheti cha Mafunzo ya Uongozi
23/8/2021	27/8/2021	MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam	Cheti cha Mafunzo ya Uongozi
6/9/2021	10/9/2021	MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam	Cheti cha Mafunzo ya Uongozi

### **Ada ya Mafunzo**

Gharama ya Mafunzo haya ni TZS 500,000/ ambayo italipwa kabla ya Mafunzo kuanza. Baada ya malipo, fedha haitaweza kurejeshwa.

### **Jinsi ya kutuma maombi**

Maombi kwa ajili ya kuhudhuria Mafunzo haya yako wazi kuanzia sasa.

Mwombaji atatuma maombi yake kwa njia ya mtandao kwa kujaza fomu iliyokatika tovuti ya Chuo ambayo ni: [www.mnma.ac.tz](http://www.mnma.ac.tz).

Mwisho wa kutuma maombi kwa ajili ya Mafunzo haya itakuwa ni wiki moja kabla ya tarehe husika ya kuanza kwa mafunzo.

### **Mawasiliano**

Kwa mawasiliano zaidi kuhusu programu hii maalumu ya Uongozi na Maadili unaweza kuwasiliana na Mratibu wa Mafunzo ya Uongozi na Maadili kupitia namba ya simu ya mkononi 255(22)2820041/47 au +255675337734: email: [kibweta@mnma.ac.tz](mailto:kibweta@mnma.ac.tz) au [rector@mnma.ac.tz](mailto:rector@mnma.ac.tz)

**Imetolewa na:**

**Mkuu wa Chuo**

**Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**